**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Mawasiliano:**

**Mkuu wa Shule; 0782177816**

**Makamu Mkuu wa Shule; 0756961623**

**Mwalimu wa taaluma; 0711967018**

**SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA CHEMBA**

**CHEMBA BOYS SECONDARY SCHOOL ,**

**S.L.P.830,**

**CHEMBA**

**Tarehe .......................**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI .................................................**
**S.L.P ...........................................................................................................**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHEMBA BOYS, HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA MKOA DODOMA MWAKA ………………………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………………………… na atasoma tahasusi ya (PCM/PCB/EGM)

**MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA**
Shule ya sekondari Chemba Boys ipo katika kijiji cha Chemba kata ya Chemba wilaya ya Chemba Shule ya ipo umbali wa Kilometa 0.5 kusini mwa Mji wa CHEMBA karibu na Chuo cha Veta Chemba.
Usafiri wa basi kutoka DODOMA mjini unapatikana kila siku kituo cha mabasi CHANG'OMBE, MACHAME NA MACHIMULAS. Nauli ni Shilingi 7,000/= Aidha unaweza kupata usafiri wa kuja Chemba kupitia Kondoa mjini ambapo kuna mabasi yanayokwenda Dodoma kupitia Chemba kila siku. Kwa anayetoka mikoani panda mabasi yanayoenda Arusha kupitia Chemba, shuka kituo cha mabasi cha Chemba.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………………

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

**SARE ZA SHULE**

i. Suruali mbili (02) au zaidi za rangi nyeusi zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) la upana wa nchi 15 (Suruali zilizobana (modo) hazitaruhusiwa) na mkanda mweusi wa ngozi. Upana wa chini ya Suruali utapimwa wakati wa kuripoti.
ii. Mashati meupe mawili (02) au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja. Mashati ya meupe ya tomato yanashauriwa zaidi. iii. Viatu vya rangi nyeusi vya kufunga na kamba na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeusi jozi mbili au zaidi.
iv. Tai ndefu rangi nyeusi (mbili)
v. Sweta na Kizibao rangi ya kijivu iliyoiva (kuna baridi kuanzia mwezi wa sita).
vi. Track suti rangi ya dark blue iliyokolea yenye ufito mweupe mikononi yenye nembo ya shule (Track suti zinapatikana kwenye maduka yaliyokaribu na shule)
vii. Sare ya kushindia (shamba dressing) Suruali ya rangi ya ugoro na T-shirt rangi ya kaki yenye nembo ya shule. (T- Shirt zinapatikana kwenye maduka yaliyo karibu na shule. Mwanafunzi anashauriwa kuwa nazo mbili)
viii. Viatu vya wazi (sandals) kwa ajili ya kushindia. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa ndala wala yeboyebo. Yeboyebo zitatumika bafuni na maliwato tu.
ix. Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo pamoja na bukta nyeusi na T shirt nyeusi jezi ya Timu ya TAIFA STARS

## 3. MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari 10 makubwa na kalamu za kutosha.
ii. Ream (A4) bunda mbili (02) uje nazo unaporipoti shuleni;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vilivyoandaliwa na TIE pamoja na vitabu vya CHANDI
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma TAHASUSI YA PCB.
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro lenye upana wa futi 2.5. unaweza kununua godoro kwenye maduka yaliyo karibu na shule.
vii. Shuka mbili (02) za rangi ya pinki, blanket 1, na chandarua kimoja cha pembe 4 rangi nyeupe
viii. Nguo za ndani za kutosha; ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2, Kubwa 1 (lita 20) na ndogo 1 (lita 10) zenye mifuniko kwaajili ya kutunzia maji.
xi. Jembe lenye mpini na ufagio mmoja wa chelewa kwaajili ya kufagilia nje, ufagio laini wa kufagilia ndani pamoja na ufagio mgumu ( hard broom yenye mipini mirefu) kwa wanafunzi wa PCB.
xii. Panga na fyekeo na mfagio mmoja wa chelewa kwaajili ya nje na mfagio laini wa ndani kwa wanafunzi wa PCM
xiii. Reki na fyekeo,pamoja na mopper yenye nyuzi(DEKIO) kwa wanafunzi wa EGM. xiv. Kitambulisho cha BIMA ya Afya cha NHIF. Ni muhimu sana matibabu ni ghali

xv. Sanduku la kutunzia vifaa vyake.

xvi. Squeezer (mpira wa kukaushia maji) 01

xvii. Koti la maabara (laboratory coat) jeupe kwaajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya vitendo (practicals) Kwa wanafunzi wa PCM/PCB xviii. Brashi ya kusugulia choo yenye mpini mfupi

xix. Jalada (file) kwaajili ya kutunzia kazi zake. Unashauriwa kuwa na jalada la nailoni au plastiki.

xx. Sabuni ya maji ya kufanyia usafi lita 5

**3. MICHANGO MBALIMBALI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- **Michango hii iwekwe kwenye akaunti ya shule yenye jina CHEMBA BOYS SECONDARY SCHOOL CAPITATION AKAUNTI, AKAUNTI NAMBA 50210051074 NMB BANK. MWANAFUNZI AJE NA BANK SLIP BAADA YA MALIPO.**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule. iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation). iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu na nywele ndefu.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote. viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. ix. Kutunza mali za shule.

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba wa mtu wa karibu au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo. iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni; xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule; xv. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

v. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHEMBA BOYS**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule MOKIWA P. JOSEPH**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO JUU YA FOMU HII**

**Fomu Na. 1**

**AHADI YA MZAZI / MLEZI**

Mimi ____________________…………………wa S.L.P__________Mji ____________Simu ________________ na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni .____________________________________natamka hapa kama mzazi / mlezi wa: __________________________.

Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Chemba Boys kuanzia tarehe _______________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahiki za kinidhamu kama alivyoorodheshewa

Jina:____________________________ saini ____________________

Tarehe: ________________ Uhusiano na mwanafunzi: ____________________

**<u>Fomu Na. 2</u>**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi ______________________________________________ Wa kidato cha Tano chaguo ~~(tahasusi) mwaka wa~~ masomo ........................... Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Chemba Boys. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:______________________________________ Saini ____________________

Tarehe: ______……………………………..

**<u>Fomu Na. 3</u>**

**KIAPO CHA MZAZI / MLEZI**

Mimi:...........................................................................................................................................
Mzazi wa:.......................................................................................................................................
S.L.P..............................Mji:.....................................................Simu............................................
Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

*Picha ya ndugu wa Kwanza*

Jina: ________________________________________ Makazi:____________ Kazi: _______________________________________

Simu:________________________________Uhusiano na mwanafunzi: _________________________

*Picha ya ndugu wa Pili*

Jina:____________________________________________________________ Kazi:____________

Makazi: _________________________ Simu: ____________________

Uhusiano na mwanafunzi:_____________________________________________________________

*Picha ya ndugu wa Tatu*

Jina:________________________________________ Kazi: ___________________

Makazi: .....................................................................Simu: _________________________________

Uhusiano na mwanafunzi:________________________________________

**Fomu Na. 4**

**CHEMBA BOYS' SECONDARY SCHOOL, P.O.BOX 830 CHEMBA**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………..…………..Age……..Sex…………year…....

1. Blood count (Red and White) ………………………………………...
2. Urinalysis Test ……………………………………………….
3. Syphilis test……………………………………………………
4. T.B.……………………………………………………………… 5. Eye Test ………………………………………………………
6. Ears……………………………………………………………
7. Spleen…………………………………………………………
8. Abdomen …………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

……………………………….. ………………………………

Name and Designation Signature and Official stamp

……………..………….………STATION DATE...........................

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.